

**HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA PWANI MHESHIMIWA  
MHANDISI EVARIST W. NDIKILO WAKATI WA MAPOKEZI YA  
MWENGE WA UHURU 2016 KUTOKA UONGOZI WA MKOA WA  
DAR ES SALAAM - TAREHE 19/05/2016**

- **Mhe. Paul Makonda-Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam,**
- Waheshimiwa Wenyeviti wa CCM Mkoa wa Pwani na Dar es Salaam,
- Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya Mikoa ya Pwani na Dar es Salaam,
- Waheshimiwa Wabunge,
- Ndugu Viongozi wa Vyama vya Siasa,
- Wajumbe wa Kamati za Ulinzi na Usalama,
- Ndugu Wakimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa,
- Ndugu Viongozi na Watendaji,
- Ndugu Wanahabari,
- Ndugu Wananchi,
- Mabibi na Mabwana.

***Amani ya Mwenyezi Mungu iwe kwenu.***

Napenda kuanza kwa kumshukuru Mungu kwa kutuwezesha kukusanyika hapa ili kukabidhiana Mwenge wa Uhuru kwa Mwaka huu wa 2016. Nawashukuru kwa dhati Wananchi na Viongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa kutukabidhi Mwenge na wakimbiza Mwenge wa Uhuru kwa wakati.

**Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa,**

Mwenge wa Uhuru utakapokuwa Mkoani Pwani utakimbizwa katika Wilaya zote sita (6) na jumla ya Miradi **47** yenye Thamani ya **Tsh 66,394,524,083 Bilioni sitini na sita, miatatu tisini na nne Milioni, Miatano Ishirini na nne elfu na**

**Themanini na tatu** itafikiwa na Mwenge wa Uhuru kwa mchanganuo ufuatao:-

- a) Miradi **14** itawekwa mawe ya msingi
- b) Miradi **11** itazinduliwa
- c) Miradi **11** itafunguliwa na
- d) Miradi **11** itakaguliwa.

**Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa na Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge,**

Miradi hiyo niliyoitaja inatekelezwa kwa ushirikiano mkubwa kati ya Wananchi na Serikali Kuu, Halmashauri, Wahisani wa Kitaifa na Kimataifa pamoja na Wawekezaji wa ndani na nje ya Nchi.

**Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa,**

Ujumbe wa Mwenge wa Uhuru mwaka huu ni:-

***Vijana ni Nguvu kazi ya Taifa,  
Washirikishwe na Kuwezesha.***

Ujumbe huu utakuwa chini ya kauli mbiu zifuatazo:-

- *Tanzania bila maambukizi mapya, unyanyapaa na vifo vitokanavyo na UKIMWI inawezekana;*
- *Tujenge jamaii, Maisha na Utu wetu; Bila Dawa za kulevya;*
- *Timiza wajibu wako; kata mnyonyoro wa rushwa.*
- *Wekeza katika Maisha ya baadaye; Tokomeza Malaria.*

**Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa,**

Katika kutekeleza ujumbe huu Mkoa wa Pwani kwa kushirikiana na Wananchi na Wadau mbalimbali umejipanga vilivyo Katika kuutekeleza ujumbe huu kwa

vitendo kama ambavyo Wakimbiza Mwenge Kitaifa watakavyojionea/shuhudia.

Aidha, sisi wananchi wa Pwani tunaamini katika kutekeleza Ujumbe wa Mwenge wa Mwaka huu kwani msingi mkubwa wa ujumbe huu ni Vijana ambao ndio nguzo na chachu kubwa ya maendeleo na nguvu kazi ya Taifa letu.

### **Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa,**

Mkoa wetu wa Pwani tuna jumla ya watu **1,098,668 (Milioni moja, elfu tisini na nane na mia sita sitini na nane)** ikiwa idadi ya Vijana wenye umri wa miaka **15-35** ni **379,646 (Laki tatu sabini na tisa elfu na miasita arobaini na sita)** sawa na **34.5%** ya watu wote wa Mkoa wa Pwani.

Kwa kutambua changamoto zinazowakabili Vijana zikiwemo za kiuchumi na kijamii Mkoa wetu umejipanga kuwasaidia Vijana katika kupunguza changamoto hizo. Aidha Miradi yetu yote imejielekeza katika kujibu changamoto zinazowakali vijana katika Mkoa wetu wa Pwani; Rai yangu ni kuwahimiza Vijana kuwajibika na kuibua changamoto zinazowakabili na kuzigeuza kuwa fursa za ajira katika maeneo yao.

### **Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa,**

Napenda kutumia fursa hii tena kukiri kuwa nimeupokea Mwenge wa Uhuru kutoka kwako ukiwa katika hali nzuri, hii ikiwa ni pamoja na vijana wetu Wakimbiza Mwenge Kitaifa.

Kwa niaba ya Wananchi wote wa Mkoa wa Pwani, ninayo heshima kubwa kuwakaribisha vijana wetu Wakimbiza Mwenge Kitaifa Mkoani Pwani na kwa kipindi chote

mtakapokuwa Mkoani kwetu mtashuhudia upendo na ukarimu wa ndugu zenu Wana-Pwani.

Kwa jirani zetu wa Dar es Salaam kwa mara nyingine tena tunawashukuru sana kwa kutukabidhi Mwenge wa Uhuru kwa wakati na niwaombe tuendeleze na kuimarisha udugu na ujirani mwema uliopo baina yetu.

Sasa tuko tayari kutekeleza jukumu la kukimbiza Mwenge Mkoani kwetu.

Karibu Mwenge wa Uhuru Mkoani Pwani.

***Tuwashirikishe Vijana katika Mipango mbalimbali ya maendeleo katika jamii zao.***

**"MUNGU IBARIKI TANZANIA"**

**"MUNGU UBARIKI MWENGE WETU WA UHURU"**

**AHSANTENI KWA KUNISIKILIZA**